

TAARIFA YA LISHE WILAYA YA MPWAPWA – ROBO YA NNE 2018/2019						
IDARA YA MAENDELEO YA JAMII						
NA	LENGO	SHUGHULI ZILIZOPANGWA	UTEKELEZAJI ROBO YA NNE HADI JUNI, 2018/2019	BAJETI ILIYOPANGWA	GHARAMA ILIYOTUMIKA	MAONI/MAELEZO
1	Kupunguza tatizo la upungufu wa wekundu wa damu kwa Wajawazito na wakina mama wanaonyonyesha na kupunguza udumavu kwa watoto chini ya miaka 2(Mkoa wa Dodoma 56% ya Watoto chini ya miaka 5 ni wadumavu)	Kuendesha mafunzo ya lishe kwa wajumbe wa Halmashauri za Vijiji 10.	Elimu ya lishe imetolewa katika jumla ya Vijiji 57 vinavyotekeleza mpango wa kunusuru kaya masikini sana ambapo jumla watu 5,808 walifikwa.	220,000.00	-	Elimu hii inahitajika sana kwa jamii yetu kutokana na wengi wao kula milo yenye aina moja ya makundi ya vyakula.Kazi hii imetekelezwa kwa kupitia fedha za TASAF na sio zile zilizotengwa kwenye bajeti ya idara kwa mwaka 2018/2019.
2		Kufanya Mikutano na Vikundi 5 vinavyojishughulisha na usindikaji katika kata 3 zenye jumla ya vijiji 10.	Utaratibu wa kukamilisha kukiunganisha kikundi cha kata ya Matomondo cha MIDO kinachojishughulisha na usindikaji wa mazao mbalimbali na Wanunuzi wa Bidhaa zao unaendelea.Utaratibu wa kusaini mikataba unaendelea ili kukiwezesha kikundi hiki kutekeleza kazi zake vizuri.	150,000.00	-	Kikundi hiki kinaendesha shughuli zake katika jumla ya Vijiji 12 vya kata za Matomondo,Mlembule,Lupeta,Kimagai,God egode,Mazae na Vig'hawe.Ushauri umetolewa ili kuwezesha kikundi hiki kuongeza eneo la utekelezaji wa kazi zake.Kazi hii iliwezesha kwa kushirikiana na MIDO.
3		Kutengeneza makaushio ya mbogamboga na kufanya maonyesho ya jinsi ya kutengeneza na kutumia katika jumla ya kata 3 zenye jumla ya vijiji 10	Kazi hii hajafanyika	244,689.09	-	Maandalizi ya utekelezaji wa kazi hii yamefanyika ikiwa ni pamoja na Utambuzi wa vikundi vyote vinavyojishughulisha na kazi za usindikaji fedha za kuwezesha kazi hii hazikutolewa.
		Kufanya uhamasishaji wa Asasi za kijamii zinzoshughulika na masuala ya lishe katika kata 5 zenye jumla ya vijiji 15	Barua za uhakiki wa Asasi zinazojishughulisha na masuala ya lishe imeandikwa kwa Viongozi wa Vijiji ili kuwezesha utaratibu wa kukutana nao.		-	Jumla ya Asasi 9 zimetambuliwa na kuonekana zinajishughulisha na kazi zinazoendana na masuala ya kuboresha lishe na hatua za kukutana nao zimeandaliwa ili kupeana maelekezo ya kutekeleza kazi hizo kwa pamoja.Asasi hizo ni pamoja na CDF,PATUA,Upendo-Nghambi,Jipe Moyo-Kiboriani,Amkeni-Igovo,Save the Children,Mshikamano-Kibakwe na Asante Tanzania cha Kizi.
4		Kuunda vikundi vya siku 1000 katika kata 10 zenye jumla ya vijiji 40	Maandalizi ya kutekeleza kazi hii yamefanyika kwa wataalamu kupata mafunzo ikiwa ni pamoja na kuandika barua kwa Watendaji wa vijiji na kata kwa ajili ya kuandaa vikundi hivi.	220,000.00	-	Kazi hii hajafanyika kutokana na kutopatolewa kwa fedha zilizokuwa zimetengwa kwenye bajeti ya 2018/2019
		Jumla Kuu Tsh.		834,689.09	-	